

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

Simu: +255 (0) 26 2322602
Tovuti: www.maji.go.tz
Barua pepe: ps@maji.go.tz



NBC Tawi la Mazengo,
Barabara ya Kuu,
S. L. P. 456,
40473 Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) amemteua Mhandisi Rejea Samweli Ng'ondya kuwa Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Mtwara (MTUWASA). Uteuzi huo unaanza leo Tarehe 12.04.2019. Mhandisi Rejea Samweli Ng'ondya kabla ya uteuzi alikua Meneja wa Mamlaka ya Maji ya Makonde, Mtwara.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) amemteua Mhandisi Charles Richard Mafie kuwa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Wizara ya Maji kuanzia leo tarehe 12.04.2019. Kabla ya uteuzi huo, Mhandisi Mafie alikua Mkuu wa Idara ya Rasilimali za Maji na Uhandisi wa Umwagiliaji katika Chuo cha Maji - Dar es salaam.

Kufuatia uteuzi huo, Waziri Prof. Mbarawa ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Wizara ya Maji Mhandisi Catherine Bamwenzaki kuanzia leo tarehe 12.04.2019 Mhandisi Bamwenzaki atapangiwa majukumu mengine.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Florence Lawrence'.

Florence Lawrence

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano.

12.04.2019